# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA

**MAKALA: OKTOBA 05, 2022**

**IMEANDALIWA NA KITENGO CHA HABARI NA MAWASILIANO SERIKALINI**

## KASI YA KIMAENDELEO LUDEWA

Mkoa wa Njombe  ni miongoni mwa Mikoa michache yenye fursa lukuki za kiuchumi ambazo zilikuwa hazitumiki ipasavyo kutokana na changamoto kubwa ya miundombinu ya barabara.

Ujenzi wa barabara ya Zege inayounganisha Wilaya ya Ludewa na Wilaya ya Njombe lakini pia inaunganisha Wilaya ya Ludewa na Wilaya ya Nyasa  imefungua fursa nyingi ikiwemo ongezeko la usafiri kutoka Wilaya moja na Wilaya nyingine, mtandao wa barabara hiyo umerahisisha usafiri na usafirishaji bidhaa hivyo kutoa fursa kwa wafanyabiashara, wakulima na wafugaji kunufaika.

Wilaya ya Ludewa tangu kuanzishwa kwa Wilaya hiyo miaka ya 1975 ilikuwa na miundombinu mbovu ya barabara kuu inayoingia na kutoka katika Wilaya hiyo.

Katika kutekeleza ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) serikali kupitia Wakala wa Barabara (TANROADS) lakini pia TARURA wamefanikiwa kuzifanyia matengenezo barabara zote kuu kwa weledi mkubwa hivyo kufungua ukurasa mpya wa uchumi wa Wilaya ya Ludewa.

Mbunge wa Jimbo la Ludewa Mhe. Joseph Kamonga nimiongoni mwa wapiganaji wanaoendelea kuwapigania wananchi haswa kupaza sauti katika kuifungua Wilaya katika kila kona za Wilaya ya Ludewa.

Mhe. Joseph Kamonga akiwa Bungeni mara nyingi hupaza sauti kwa kilio cha wananchi haswa katika miundombinu ya barabara, Mawasiliano, Elimu, Maji lakini pia katika fursa za Uwekezaji.

Mbunge huyo akihojiwa na vyombo mbalimbali vya habari amekuwa akieleza mengi na hapa alisema, uwekezaji ambao umeanza kushika kasi Wilayani Ludewa utokanao na Makaa ya mawe utawafanya wananchi wa Wilaya hiyo kubadilisha maisha yao kwa kufanya biashara ya vyakula, Malazi lakini pia ongezeko la ajira katika sekta zote na mara nyingi amenukuliwa akimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha ya Ujenzi wa Chuo kikubwa cha Ufundi stadi VETA katika Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

**Hali ya barabara kwa sasa**

Barabara zote zinazounganisha Wilaya na Kata kwa Kata sasa zimetengenezwa kwa kiwango kizuri hivyo ukitoka kata moja na nyingine ni rahisi ukilinganisha na miaka mingine iliyopita.



Kilomita 50 za ujenzi wa barabara hiyo ya Zege zimekamilika na kwasasa barabara hiyo tayari inatumika ikiwa ipo hatua za mwisho za umaliziaji.

**Barabara zinazoendelea na Ujenzi**

Serikali imeendelea kutoa fedha za ujenzi wa barabara Wilayani Ludewa ikiwa ni pamoja na barabara ya Lami ya kutoka Ludewa mijini kwenda Manda ambayo inajengwa kwa Lami Kilomota 2.5 barabara yakutoka Ludewa Mjini kwenda Lupingu sambamba na hizo serikali imeendelea kujenga barabara zingine nyingi ikiwemo barabara ya Mbwila hadi Lifuma.

Aidha Mheshimiwa Mbunge amehakikisha sehemu korofi kwenye barabara kubwa zote zinafanyiwa marekebisho kabla msimu wa masika haujawadia, kupitia TARURA amehakikisha ujenzi wa eneo la Kilulu barabara ya Madilu – Ilininda kwa mfumo wa reli (concrete strips)



Pia barabara ya Muholo – Lugarawa inayo unganisha kata nne za Luana, Ludende, Mkongobaki na Lugarawa umekamilika na sasa inapitika vizuri.

Mhe. Mbunge amefanya ufuatiliaji wa karibu juu ya ujenzi wa daraja la mto Ruhuhu linalo unganisha wilaya ya Ludewa na wilaya ya Nyasa mkoa wa Ruvuma limekamilika na linatoa huduma kwa wananchi.

Upande wa Idara ya maji Mbunge hajaiacha nyuma kwani kwa sasa ujenzi wa tenki la maji la lita laki tano lipo hatua za mwisho upakaji wa rangi likisha kamilika litamaliza adha ya maji Ludewa mjini lakini pia matenki ya zamani yamefanyiwa ukarabati na yanaendelea kutoa huduma, kuna miradi mingine ya maji inaendelea kutekelezwa sehemu tofautitofauti mfano mradi wa maji kata ya Madope na mradi wa maji kata ya Mawengi.




Hili ni tenk kubwa la Maji lilipo katika Kijiji cha Ludewa Mjini Kata ya Ludewa, Tenki hili litahudumia watanzania wote wanaoishi maeneo yote ya Kijiji cha Ludewa mjini na kuongeza nguvu katika kijiji cha Ludewa kijijini yapata lita laki tano ndizo zitakazo hifadhiwa katika tenki hili na kilio cha wananchi katika adha ya maji itakuwa imemalizika, Kukamilika kwa tenki hili nisehem ya miundombinu inayoendelea kujengwa kutokana na chanzo kipya cha Ilunga, gharama za mradi wa wote unategemea kughalimu Bilioni 7.4

Pamoja na ukiondoa Miradi midogo mingi ya maji basi hapa nakuangazia Miradi mikubwa ya maji ukianza na mradi wa ujenzi wa mradi wa Maji Mjini, Ujenzi wa Mradi wa maji Katika kata ya Mawengi ambao unagharimu zaidi bilioni moja na mradi mwingine mkubwa wa maji uliokamilika ni wa Kata ya Madope ambao umegharimu Milioni 500.

Ikumbukwe kwamba ni miaka mingi imepita Kata ya Manda ilikuwa inakumbwa na changamoto kubwa ya maji, hivi karibuni Mbunge wa Jimbo la Ludewa alipaza sauti na kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025 nakufanikisha utekelezaji wa Miradi ya maji ya kijiji cha Nsungu na Mbongo ambapo tayari Pampu za kusukuma maji kupeleka kwenye tenki tayari zimefungwa.

Kwa upande wa Kata ya Lupingu ambapo mvua nyingi zilizoathiri miundombinu ya maji ikiwemo kata ya Lupingu sasa kilio cha muda mrefu kinakwenda kumalizika kwasababu tayari tenda imetangazwa ili maboresho na urejeshwaji wa maji katika kata hiyo unaendelea.

Kwaupande wa sekta ya Mawasiliano ndani ya Kata za Wilaya ya Ludewa zinaendelea kutatuliwa ikiwa ni pamoja na kuwashwa kwa minara mipya ya mitandao ya simu katika kata zifuatazo, 1. Kata ya Nkomang'ombe 2. Kata ya Ibumi 3. Kata ya Lupanga 4. Kata ya Mkongobaki 5. Kata ya Madilu 6. Kata ya Madope na Kata ya Lupingu.

Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa imepokea kiasi cha Bilioni 2.6 hizi zote ni juhudi na muunganiko wa viongozi wote wa Wilaya ya Ludewa na ni matunda ya juhudi za Mbunge akiwa anawapigania wananchi wa Wilaya ya Ludewa akiwa ndani na nje ya Bunge yanadhihilika kwa vitendo kwani mpaka sasa tayari fedha zilizo ifikia wilaya ya ludewa ni pamoja na :-



- Jengo la utawala 900,000,000
- Hospitali 900,000,000
- Ujenzi wa Nyumba ya Mkurugenzi 150,000,000
- Ukamilshaji zahanati 100,000,000
- Ukamilishaji Madarasa Msingi 118,750,000
- Ujenzi nyumba za walimu mazingira magumu 200,000,000
- Ukamilishaji wa bwalo shule ya sekondari ya Mundindi 50,000,000
- Ukamilishaji wa bweni shule ya sekondari ya Mchuchuma 20,000,000
- Ukamilishaji wa bweni Elimu maalumu 20,000,000
- Ujenzi wa uzio Elimu maalumu 30,000,000

**Mkuu wa Wilaya ampongeza Rais Samia Suluhu Hassan**

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Mhe. Andrea Tsere anampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa awamu ya 6 Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia fedha za kutosha kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta zote.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Mhe. Wise Mgina ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Mundindi anaeleza kuwa sasa hawana shida ya usafiri kama ilivyokuwa zamani,

kwani wafanyabiashara na wakulima hawahangaiki tena kusafiri bidhaa na mazao yao.

Vasco Mgimba ambaye ni Diwani wa Kata ya Ludende anamshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwajengea barabara ya kisasa na kuwapatia fedha ya kutekeleza Miradi mikubwa ikiwemo ya Kituo cha Afya cha Mundindi lakini pia uboreshaji wa Hospitali ya Wilaya.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Sunday Deogratias anawakaribisha wawekezaji kutoka maeneo yote ya Tanzania na nje ya mipaka ya Tanzania kuja kuwekeza katika Halmashauria ya Wilaya ya Ludewa na anaipongeza serikali kwa kazi kubwa inayofanya ya kuufungua Wilaya hiyo na kuifanya Wilaya hiyo kuwa miongoni mwa Wilaya inayovutia wawekezaji wengi.

Anatoa wito kwa Wawekezaji wa ndani ya nje ya nchi kuja kutembelea Wilaya ya Ludewa ili watazame na kujionea fursa mbalimbali ikiwemo mazingira mazuri ya uwekezaji katika sekta zote.

Mimi Chrispin Bernad Kalinga naomba kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia fedha Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ya kutekeleza Miradi mbalimbali.

Sambamba na hayo naomba nimpongeze kwa kuiongoza nchi yetu kwa umahiri mkubwa na kudumisha Amani, Upendo, Utulivu na Mshikamano.

